

RECEIVED
29 AUG 2017
MIPINDWE DISTRICT COUNCIL

JAMHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA KATAVI

Anuani ya simu: "REGCOM"
Simu Na: (025)
Fax Na. (025)
Unapojibu tafadhali taja:



OFISI YA MKUU WA WILAYA
WILAYA YA MLELE,
S. L. P. 471,
MPANDA.

Kumb. Na. CAB.63/348/01/122

01/08/2016

**WANANCHI WOTE
WILAYA YA MLELE**

**MAAFISA TARAFU
WILAYA YA MLELE**

**WATENDAJI WA KATA
WILAYA YA MLELE**

**WATENDAJI WA VIJIJI
WILAYA YA MLELE**

AMRI HALALI NO 1/2016 YA MKUU WA WILAYA YA MLELE

Mimi Mkuu wa Wilaya ya Mlele kwa Mamlaka niliyopewa na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Mamlaka ya Mkuu wa Wilaya Na. 466 ya mwaka 1962 Kifungu cha 89 (C) na Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 9 ya mwaka 1997 kifungu cha 15 (I) Na. (2) leo tarehe 01/08/2016 natangaza **AMRI HALALI NO 1/2016** itakayoanza kutumika kuanzia tarehe 15/08/2016 katika kipindi cha miaka mitano hadi tarehe 15/08/2020.

AMRI HII HALALI ISOMEKE KAMA IFUATAVYO

1. Kila Mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi na afanye kazi ya kumpatia kipato halali.
2. Kila Mwananchi ashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Atakaye kaidi kushiriki shughuli za maendeleo achukuliwe hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa

3. Kila Mwananchi afuate sheria zote za nchi.
4. Kila Mwananchi ahakikishe anatumza mazingira na kusafisha eneo lake anakoishi endapo itakutwa eneo lake ni chafu faini ya papo kwa papo itatozwa ya Tsh. 50,000/= na inaweza kuwa kubwa kutokana na wingi wa uchafu.
5. Kila Mwananchi ahakikishe hatupi taka ovyo na hajisaidii ovyo barabarani akikutwa anatupa taka au anajisaidia ovyo atatozwa faini ya shilingi 50,000/= papo hapo.
6. Kila Kaya iwe na choo bora na ikibainika Kaya haina choo itatozwa faini ya shilingi 50,000/= papo hapo.
7. Kila Alhamisi ya kila wiki na Jumamosi ya mwisho wa mwezi ni siku ya Operesheni maalum ya Safisha Wilaya ya Mlele kila Mwananchi atatakiwa na uongozi wa Serikali ya Mtaa/Kijiji kushiriki. Ni marufuku kwa siku hizo kufanya shughuli za biashara kuanzia saa 12.00 hadi saa 4.00 asubuhi isipokuwa maduka ya madawa ya binadamu atakaye kaidi au kuanza kufanya biashara kabla ya wakati atatozwa faini ya Tshs. 50,000/= papo hapo.
8. Ni marufuku kwa maeneo yote ya starehe na vilabu vya pombe aina zote kufunguliwa kabla ya saa 9.30 alasiri kwa siku za kazi akikutwa muuzaji au mnywaji atatozwa faini ya Tsh. 50,000/= papo hapo. Pia ni marufuku kupiga muziki baada ya saa 6.00 kwa siku za mwisho wa wiki na siku za kawaida mwisho ni saa 5:00 usiku atakayekutwa anafungua biashara atatozwa faini ya Tsh. 200,000/= papo hapo na hatua za kisheria zinafuatwa.
9. Ni marufuku wananchi kukaa kwenye vijiwe vya kahawa au kucheza bao, pool au draft kabla ya saa 9:30 alasili akikutwa anatozwa faini 50,000/= papo hapo.
10. Ni marufuku kwa mifugo ya aina yoyote kuzurura hovyoyote mitaani atakayekutwa faini ya kila mfugo atatozwa ng'ombe 50,000/=, Kondoo na Mbuzi 20,000/= na nguruwe 30,000/=
11. Kila Mtoto aliye na umri wa kwenda Shule aandikishwe Shule na kuanza masomo mara moja.
12. Msimu wa kilimo kila Mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi atatakiwa alime angalau ekari moja ya mazao ya chakula na ekari moja ya mazao ya biashara.
13. Magari makubwa hayaruhusiwi kuegeshwa katikati ya mji wa Inyonga.
14. Ni marufuku kupiga muziki wa watoto (disco toto) ndani ya ukumbi, muziki huo upigwe kwenye maeneo ya wazi na rafiki kwa watoto kuanzia saa 8:00 hadi saa 12:00
15. Ni marufuku watoto wadogo wenye umri wa kwenda shule kuchunga mifugo siku za masomo, mtoto atakayekutwa anachunga mifugo siku za masomo, mzazi wa mtoto atatozwa faini ya Tshs. 50,000.00 papo hapo na hatua za kisheria zitafuata.

16. Yeyote atakayekluka **AMRI HALALI HII** akamatwe na achukuliwe hatua kali za kisheria.



Rachel Stephen Kassanda

MKUU WA WILAYA

MLELE
MLELE
MLELE

Nakala:-

RC -	KATAVI	-	Kwa taarifa
DSO -	MLELE	-	Kwa taarifa
OCD -	MLELE	-	Kwa taarifa
DED -	MLELE	-	Kwa taarifa
DED -	MPIMBWE	-	Kwa taarifa
MJA -	MLELE	-	Kwa taarifa
DIO -	MLELE	-	Kwa taarifa
PCCB W	MLELE	-	Kwa taarifa
Meneja TFS	MLELE	-	Kwa taarifa
Meneja pori RUKWA/LWAFI-		-	Kwa taarifa
Mhifadhi Mkuu KATAVI		-	Kwa taarifa
Hakimu Mfawidhi		-	
Mahakama ya Mwanzo		-	Kwa taarifa
Inyonga na Usevya		-	